



**Vodacom Tanzania Public Limited Company**

(Imesajiliwa katika Jamhuri ya Muungano wa Tanzania)

(Namba ya Usajili 38501)

(ISIN: TZ1996102715 Code ya Tiketi: VODA)

('Vodacom Tanzania' au 'Kampuni')

**Kujiuzulu kwa Mkurugenzi Huru**

Bodi ya Wakurugenzi ya Vodacom Tanzania inatangaza kujiuzulu kwa Jaji (Mstaafu) Thomas B Mihayo, kama Mkurugenzi Huru na Mwenyekiti wa Bodi ya Wakurugenzi na Kamati ya Uteuzi, kuanzia Aprili 1, 2025, ili kujikita katika shughuli binafsi.

Jaji Mihayo ameonyesha uongozi thabiti unaoendana na maono na maadili ya kampuni. Katika uongozi wake, amekuwa kiungo muhimu kwenye ukuaji na mafanikio ya Kampuni. Bodi inachukua fursa hii kumpongeza kwa huduma na uongozi uliotukuka. Tunamtakia kila la heri katika shughuli zake zijazo.

Bodi inaendelea na mchakato wa kumpata Mwenyekiti mpya na taarifa zaidi zitatolewa katika muda muafaka.

Kwa idhini ya Bodi.

A handwritten signature in black ink, appearing to read 'Caroline Mduma', written over a horizontal line.

**Caroline Mduma**

Katibu wa Kampuni

22 Novemba 2024

**Together we can**